MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA

JARIDA LA HALI YA HEWA

Na. 26 Toleo Maalum: Utabiri wa mvua za Novemba hadi Aprili (NDJFMA) 2021/ 2022 Limetolewa tarehe, 27 Oktoba, 2020

MUHTASARI

- Utabiri wa mvua za mwezi Novemba hadi Aprili (NDJFMA) ni mahususi kwa maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka.
- Mvua zinatarajiwa kuwa za chini ya wastani hadi wastani katika maeneo mengi ya mikoa ya Kigoma, Tabora, Katavi, Singida, Dodoma, Rukwa, Songwe, Mbeya na Iringa na wastani hadi chini ya wastani katika baadhi ya maeneo ya mikoa ya Njombe, Ruvuma, Lindi, Mtwara na kusini mwa mkoa wa Morogoro.
- Vipindi virefu vya ukavu vinatarajiwa kati ya mwezi Novemba, 2021 na Januari, 2022.
- Mvua zinatarajiwa kuanza katika wiki ya tatu ya mwezi Novemba, 2021 katika maeneo mengi na kuisha kati ya wiki ya pili na ya tatu ya mwezi Aprili, 2022.
- Malisho na maji ya mifugo vinatarajiwa kupungua hivyo kupelekea kongezeka kwa migororo ya wakulima na wafugaji.

MWELEKEO WA MIFUMO YA HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA NDJFMA, 2021/2022

Hali ya sasa ya joto la bahari katika eneo la kati la bahari ya Pasifiki joto liko chini ya wastani na inatarajiwa kuendelea kuwa chini ya wastani katika nusu ya kwanza ya msimu ingawa inatarajiwa kuongezeka hasa katika nusu ya pili ya msimu. Joto la bahari la mashariki mwa bahari ya Hindi (Indonesia) linatarajiwa kuwa juu ya wastani ukilinganisha na eneo la magharibi mwa bahari ya Hindi (pwani ya Afrika Mashariki). Joto la bahari la chini ya wastani linatarajiwa katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi hususan katika kipindi cha nusu ya kwanza ya msimu, na juu ya wastani katika nusu ya pili ya msimu. Hali hiyo inatarajiwa kupunguza uwezekano wa kutokea kwa migandamizo midogo ya hewa na hivyo kucheleweshа mifumo inayosababisha mvua katika maeneo ya kusini mwa nchi hususan katika kipindi cha nusu ya kwanza ya msimu. Joto la bahari linatarajiwa kuwa la wastani katika eneo la mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na Pwani ya Angola). Kwa ujumla mifumo ya hali ya hewa inayotarajiwa inaweza kudhoofisha mifumo inayosababisha mvua katika baadhi ya maeneo ya nchi hususan magharibi, kusini na kanda ya kati.

MWELEKEO WA MVUA ZA MSIMU, NDJFMA 2021/2022

Mvua za *Msimu* ni mahususi katika maeneo ya magharibi mwa nchi, kanda ya kati, nyanda za juu kusini magharibi, pwani ya kusini na mikoa ya kusini mwa nchi. Maeneo haya yanapata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka, unaoanza mwezi Novemba hadi Aprili ya mwaka unaofuata.

Kutokana na mifumo ya hali ya hewa inayotarajiwa, mvua za chini ya wastani hadi wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya mikoa ya Kigoma, Tabora, Katavi, Singida, Dodoma, Rukwa, Songwe, Mbeya na Iringa. Aidha, mvua za wastani hadi chini ya wastani zinatarajiwa katika baadhi ya maeneo ya mikoa ya Njombe, Ruvuma, Lindi, Mtwara na kusini mwa Morogoro. Katika nusu ya kwanza ya msimu (Novemba - Januari) vipindi virefu vya ukavu vinatarajiwa. Hata hivyo, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa mwezi Machi, 2022 katika nusu ya pili ya msimu. Maelezo ya kina juu ya mwelekeo wa mvua hizo za msimu ni kama ifuatavyo:

Kanda ya magharibi (mikoa ya Kigoma, Tabora na Katavi): Mvua za chini ya wastani hadi wastani zinatarajiwa katika mikoa ya Kigoma, Tabora na Katavi. Mvua hizo

zinatarajiwa kuanza katika wiki ya tatu ya mwezi Novemba, 2021 katika maeneo mengi. Mvua hizo zinatarajiwa kuisha wiki ya pili ya mwezi Aprili, 2022 katika mkoa wa Katavi na wiki ya tatu ya mwezi Aprili, 2022 katika maeneo mengine yaliyosalia.

Kanda ya Kati*: *(mikoa ya Singida na Dodoma): Mvua katika maeneo haya zinatarajiwa kuwa za chini ya wastani hadi wastani na zinatarajiwa kuanza kati ya wiki ya pili na ya tatu ya mwezi Disemba, 2021. Mvua zinatarajiwa kuisha wiki ya tatu ya mwezi Aprili, 2022.

Nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Iringa, Njombe, pamoja na maeneo ya kusini mwa mkoa wa Morogoro):
Mvua za chini ya wastani hadi wastani zinatarajiwa katika maeneo ya mikoa ya Rukwa, Iringa, Songwe na Mbeya. Aidha, mvua za wastani hadi chini ya wastani zinatarajiwa katika mikoa ya Njombe, kusini mwa Morogoro na maeneo ya miinuko ya mkoa wa Mbeya. Mvua katika maeneo haya zinatarajiwa kuanza kati ya wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Novemba, 2021 na kuisha katika wiki ya tatu ya mwezi Aprili, 2022. Hata hivyo, maeneo ya kusini mwa mkoa wa Morogoro mvua zinatarajiwa kuanza wiki ya pili ya mwezi Novemba, 2021 na kuisha wiki ya kwanza ya mwezi Aprili, 2022.

Pwani ya kusini na maeneo ya kusini mwa nchi (mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma):
Mvua za wastani hadi chini ya wastani zinatarajiwa katika maeneo ya mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma. Mvua zinatarajiwa kuanza wiki ya pili ya mwezi Novemba, 2021 katika mikoa ya Lindi na Mtwara na wiki ya tatu ya mwezi Novemba, 2021 katika mkoa wa Ruvuma. Mvua zinatarajiwa kuisha katika wiki ya nne ya mwezi Machi, 2022 katika mkoa wa Ruvuma na wiki ya pili ya mwezi Aprili, 2022 katika mikoa ya Lindi na Mtwara.
Aidha, upo uwezekano wa kutokea kwa mgandamizo mdogo wa hewa kaskazini mashariki mwa kisiwa cha Madagascar, hivyo kusababisha kurejea kwa mvua katika baadhi ya maeneo mwishoni mwa mwezi, Aprili, 2022.



Kielelezo: Mwelekeo wa mvua za *Msimu,* NDJFMA 2021/2022

ATHARI NA USHAURI

Kilimo, Mifugo, Uvuvi na Wanyamapori

Mvua za chini ya wastani hadi wastani zinazotarajiwa katika maeneo mengi yanayopata mvua za msimu, zitapelekea upungufu mkubwa wa unyevunyevu katika udongo na kuathiri ukuaji wa mazao. Aidha, ongezeko la visumbufu vya mazao kama mchwa, viwavijeshi, panya na magonjwa vinatarajiwa kujitokeza katika msimu na hivyo kuathiri mazao na uzalishaji kwa ujumla. Hali kadhalika uzalishaji wa asali unatarajiwa kuathirika kutokana na upungufu wa maji na maua. Wakulima wanashauriwa kupanda mazao na mbegu zinazokomaa ndani ya muda mfupi na zinazostahimili mvua chache kama vile mazao jamii ya mizizi na mazao ya bustani.

Upatikanaji wa maji na malisho kwa ajili ya mifugo vinaweza kuathirika na kupelekea uwezekano wa migogoro kujitokeza baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi. Aidha, baadhi ya magonjwa ya mifugo (yanayoenezwa na kupe pamoja na wadudu warukao), uzalishaji wa mifugo na mazao ya mifugo unatarajiwa kupungua. Pia, upatikanaji wa chakula kwa ajili ya samaki unatarajiwa kupungua na kuathiri mazao ya samaki. Hali ya ongezeko la joto inaweza kujitokeza na kusababisha vimelea vya magonjwa mbalimbali ya samaki. Kwa upande mwingine kilimo cha mwani katika maji ya kina kifupi kinatarajiwa kuathirika kutokana na vipindi virefu vya ukavu vinavyotarajiwa. Aidha, Wakulima wa mwani katika mikoa ya Lindi na Mtwara wanashauriwa kupanda aina ya mbegu zinazostawi kwenye maji ya kina kirefu.

Hali ya malisho na maji kwa wanyamapori inatarajiwa kupungua kutokana na mtawanyiko hafifu wa mvua unaotarajiwa. Hali hii inaweza kusababisha migogoro baina ya wanyamapori na jamii inayozunguka hifadhi za wanyamapori. Aidha, kusambaa kwa magonjwa ya mlipuko kwa wanyama wanaofugwa na wanyamapori kunaweza kujitokeza kutokana na mwingiliano wakati wa kutafuta maji na malisho. Mamlaka husika zinashauriwa kuboresha miundombinu ya usafirishaji katika hifadhi za wanyamapori na kujenga uelewa kwa jamii pamoja na kuchukua hatua stahiki. Aidha, jamii inashauriwa kutoa taarifa kwa Mamlaka husika pindi kunapokua na uvamizi wa wanyamapori katika makazi.

Sekta ya Maji

Mtiririko wa maji katika mito, kina cha maji katika mabwawa na hifadhi ya maji ardhini vinatarajiwa kupungua hususan katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za chini ya wastani. Hali hii inaweza kupunguza upatikanaji wa maji kwa matumizi mbalimbali na kupelekea migogoro baina ya watumiaji wakubwa na wadogo.

Wadau wanashauriwa kuzingatia matumizi endelevu ya maji katika shughuli zao. Vilevile, Sekta husika ziendelee kufuatilia tabiri zitolewazo na Mamlaka ya Hali ya Hewa Nchini.

Menejimenti ya Maafa

Katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za chini ya wastani hadi wastani, madhara yanayoweza kujitokeza ni pamoja na upungufu wa uzalishaji wa mazao ya chakula, malisho ya mifugo na maji. Mamlaka husika na kamati za usimamizi wa maafa katika ngazi ya mkoa, wilaya, kata na vijiji zinashauriwa kushirikiana na kuchukua hatua stahiki ikiwemo kutoa elimu na miongozo itakayohamasisha uhifadhi wa chakula, maji na malisho ya mifugo.

Zingatio 1: Izingatiwe kuwa matukio ya vipindi vifupi vya mvua kubwa yanaweza kujitokeza hata katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za chini ya wastani.

Zingatio 2: Mwelekeo wa mvua uliotolewa umezingatia zaidi kipindi cha msimu (miezi sita) na hali ya mvua katika maeneo makubwa. Hivyo, viashiria vinavyochangia mwenendo wa mifumo ya mvua na mabadiliko ya muda mfupi katika maeneo madogo vitazingatiwa katika uchambuzi wa utabiri wa muda wa kati na mfupi. Watumiaji wa taarifa za utabiri huu wanashauriwa pia kufuatilia utabiri wa saa 24, siku 10 pamoja na mwezi kama unavyotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.

Jarida limetayarishwa na:

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania

Ghorofa ya 3 -Ubungo Plaza – 388 Barabara ya Morogoro,

S.L.P 3056; 16102 Dar es Salaam, Simu. 255 -(0) 22 – 2460706-8; Nukushi: 255 - (0) 22 – 2460718 ; Barua pepe: (1) met@meteo.go.tz (2) agromet@meteo.go.tz; Tovuti:

www.meteo.go.tz, -Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania